LIC | LOCAL INVESTMENT CLIMATE

**Brief No. 5**

# UWEKEZAJI WA PAMOJA KATI YASEKTA YA UMMA NA SEKTA BINAFSI KWA AJILI YA MAENDELEO YA BIASHARA

Mradi wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji (LIC) ni mradi wa kuendeleza sekta binafsi unaofadhiliwa na Danida. Mradi unashughulikia vikwazo vikuu vinavyokwamisha maendeleo ya biashara na ukuaji wa uchumi katika ngazi ya wilaya kwenye mikoa miwili ya Dodoma na Kigoma nchini Tanzania. LIC imejikita katika mijadala kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, miundombinu ya utoaji wa huduma za biashara ikiwa ni pamoja na vituo vya pamoja vya biashara na miundombinu ya pamoja kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ili kusaidia maendeleo ya biashara na uwekezaji. Washirika wanaotekeleza mradi wa LIC ni Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Sekretariati za mikoa ya Kigoma na Dodoma, Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) Tanzania, Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT), Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Chemba ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA).

LIC ilianza shughuli zake mnamo mwaka 2014 na programu imepata maarifa na uzoefu mkubwa wa changamoto na vikwazo vinavyokwamisha maendeleo ya biashara. Ushirikiano wa karibu na washirika wa mradi umechangia kupata mafunzo mazuri yatokanayo na mradi na kuwezesha LIC kuchangia kwenye uundaji wa mikakati na sera mpya za maendeleo ya sekta binafsi.

Lengo la LIC ni kufikia mageuzi ya kiuhalisia yatakayobadilisha mwenendo wa shughuli za biashara na uchumi katika ngazi ya mamlaka za serikali za mitaa, kupunguza gharama na vikwazo vinavyoweza kuathiri shughuli za biashara na kuboresha ushindani wa sekta binafsi na vyanzo vya mapato vya serikali za mitaa.

**Uwekezaji wa LIC katika kusaidia mazingira ya biashara**

LIC imesaidia ukarabati wa maeneo ya masoko, minada, machinjio, mialo ya samaki, miradi ya umwagiliaji, kituo cha mafunzo ya kilimo, mifumo ya kusambaza maji na vifaa vya usindikaji mdogo. Uwekezaji wote huu unalenga kushughulikia vikwazo vya biashara kama vilivyoainishwa kupitia majadiliano kati sekta ya umma na sekta binafsi ambayo pia yanafadhiliwa na LIC kupitia kuanzishwa kwa mabaraza ya biashara ya wilaya katika wilaya zote za mikoa ya Dodoma na Kigoma na mabaraza ya biashara katika mikoa hiyo miwili.

Msaada wa LIC kwa sekta ya umma katika uwekezaji wa miundombinu ya biashara unahitaji ufadhili wa pamoja wa asilimia 20 kutoka serikali za mitaa na kwa upande wa sekta binafsi ni asilimia 50. Kabla ya kufanya uwekezaji, LIC inafanya uchambuzi wa kibiashara pamoja na kusaidia kuanzisha mipango ya biashara.





Soko la usiku la Mwanga, Kigoma Ujiji.

**Changamoto katika uwekezaji wa pamoja kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPP).**

Baadhi ya changamoto kuu zinazofanya uwekezaji endelevu kuwa katika hatari ya kutofanikiwa katika uwekezaji unaosimamiwa na serikali za mitaa:

1. Uelewa mdogo wa mahitaji na mwenendo wa biashara
2. Uelewa mdogo wa kanuni za uwekezaji wa pamoja kati ya sekta ya umma na sekta binafsi na upana wake
3. Uwezo mdogo wa kuandaa na kutekeleza miradi ya uwekezaji
4. Uwezo mdogo wa kusimamia nyenzo za uwekezaji wa pamoja kati ya sekta ya umma na sekta binafsi
5. Ugumu mkubwa katika kuchangia asilimia 20 kutoka sekta ya umma ya ufadhili wa pamoja wa miradi

Kutokana na athari za changamoto hizi uwekezaji wa LIC kiujumla unakabiliana na ucheleweshaji katika kuandaa, kutekeleza na kumaliza miradi. Mbali zaidi, maombi ya kurejeshwa fedha zilizotengwa kutokana na kutofanya vizuri kulingana na makubaliano ya uwekezaji na mchango wa asilimia 20 ambao serikali ya mtaa ilipaswa kutoka mara kadhaa imekuwa ikitolewa na mradi wa LIC ili kuweza kulinda uwekezaji wa asilimia 80 ambao mradi unakuwa umeshachangia.

Mradi wa LIC unatambua ufinyu wa bajeti unazikabili serikali za mitaa pamoja na upungufu wa rasilimali watu. Ukizingatia umuhimu wa uwekezaji wa pamoja kati ya sekta ya umma na sekta binafsi katika kusaidia maendeleo ya biashara na kutambua kwamba vikwazo hivi vinavyozikabili serikali za mitaa havitoweza kubadilika kwa kasi kwa kipindi cha miaka michache ijayo, uzoefu wa mradi wa LIC unapendekeza kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika kusimamia na kutekeleza uwekezaji kupitia chombo au mfumo wa SPV.





Mwalo wa Kibirizi na soko la samaki, Kigoma Ujiji.

**Dhana ya SPV kama chombo cha usimamizi**

Chombo hichi kinachoitwa SPV kimekuwa kikitumika kwa ufanisi kusimamia miradi ya pamoja kati ya sekta ya umma na sekta binafsi. Kampuni binafsi yenye ukomo wa dhamana inaanzishwa kusimamia uwekezaji na kukusanya mapato kufuatana na taratibu au sheria ndogo za serikali. Kampuni inawajibika na majukumu yote yanayohusiana na shughuli za uendeshaji na ukarabati na pia inawajibika kwa bodi ya wakurugenzi inayoundwa na wadau kutoka sekta ya umma na sekta binafsi. Kilichoanzishwa kitaendelea kuwa mali ya mamlaka ya serikali ya mtaa na kampuni ya SPV itaongozwa na mkataba wa makubaliano na mamlaka ya serikali ya mtaa.

Mbali na kuchukua ujuzi wa sekta binafsi katika usimamizi, bodi ya SPV inaweza kuleta kundi pana la wadau ili kuhakikisha upatikanaji wa msaada mpana kwenye uwekezaji na makusanyo ya mapato huku utoaji huduma ukiimarika.

Mbali na hayo, utaratibu wa kutumia SPV unawezesha kampuni inayoendeshwa kwa utaratibu huu kukopesheka kwa sababu itakuwa inazingitia makubaliano ya mpango wa biashara

**Chaguzi ya jinsi ya kuendelea**

1. SPV kuanzishwa kama chombo halali kilichoidhinishwa kisheria kikiwa na miongozo ya uendeshaji tayari kwa usajili na utekelezaji
2. Bodi ya wakurugenzi kujumuisha serikali za mtaa, serikali ya mkoa na wawakilishi kutoka ngazi ya kijiji, wakulima/wazalishaji, vijana, wanawake, na makundi maalumu kwa uwekezaji wowote wa pamoja kati ya serikali na sekta binafsi
3. Utekelezaji wa SPV utakuwa ni hatua ya kwanza katika uwekezaji wa pamoja kati ya serikali na sekta binafsi na mwendelezo wa shughuli zote za uwekezaji ukijumuisha mipango, makadirio ya gharama za ujenzi, zabuni, mikataba nk. Usimamizi wa ujenzi na uendeshaji wa uwekezaji utafanywa na kampuni ya SPV. Wafanyakazi wa serikali wa eneo husika watakuwa waangalizi wa kampuni ya SPV kwa niaba ya bodi ya wakurugenzi
4. Kwa kuwa SPV inatarajiwa kuwa inakopesheka, asilimia 20 ya fedha ya mchango wa uwekezaji katika miradi ambayo inatakiwa kutolewa na mamlaka za serikali za mitaa itatolewa na benki/LIC kama mkopo kwa SPV na italipwa katika mfuko utakaotumika kwa ajili ya maendeleo ya Kongano. Mfuko huo utasimamiwa na bodi ya SPV kwa kuzingatia mikakati na miongozo itayowekwa na bodi

LIC imewekeza takriban kiasi cha shilingi bilioni 5.7 za kitanzania katika miradi ya pamoja kati ya umma na sekta binafsi.

Kwa taarifa zaidi, tafadhali temebelea tovuti ya mradi wa LIC: www.lic.or.tz

**Oktoba 2018**